

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Tele: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge
S.L.P. 941
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkutano wa Kumi wa Bunge unatarajiwa kuanza siku ya Jumanne tarehe 30 Januari 2018 na kumalizika tarehe 9 Februari 2018 Mjini Dodoma. Shughuli zitakazofanyika katika Mkutano huu ni kama ifuatavyo:-

1.0 KIAPO CHA UAMINIFU

Kutakuwa na Kiapo cha Uaminifu kwa Waheshimiwa Wabunge wapya wafuatao :-

- i. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro – Songea Mjini.
- ii. Mhe. Monko Justine Joseph – Singida Kaskazini.
- iii. Mhe. Dkt. Stephano Lemomo Kiruswa – Longido.

2.0 MASWALI

Katika Mkutano huu wa Kumi, wastani wa maswali 125 ya Kawaida yanatarajiwa kuulizwa na Wabunge. Aidha, wastani wa Maswali 16 ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yanatarajiwa kuulizwa kwa siku ya Alhamisi tarehe 1 na 8 Februari, 2018.

3.0 MISWADA YA SERIKALI

Bunge pia linatarajia kupitisha kwa hatua zake zote Miswada Miwili ya Sheria ambayo ilisomwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 91. Miswada hiyo ni :-

- i. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 **[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017]**.
- ii. Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 **[The Public Service Social Security Fund Bill, 2017]**.

4.0 TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE

Aidha, Kamati 16 za Kudumu za Bunge zitawasilisha Taarifa zake Bungeni.

Ratiba yote ya Mkutano wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz.

Imetolewana:

Kitengo cha Habari, Elimuna/Mawasiliano
Ofisi ya Bunge
DODOMA
29 Januari, 2018.